

Ujinsia na Wajibu wa Binadamu

Barua ya Idhini

Afya ya Shule ya Sekondari

Mzazi au Mlezi,

Kwa kuzingatia Sera ya Bodi ya Austin ISD EHAA (Austin ISD Board Policy EHAA), mtaala wa Ujinsia na Wajibu wa Binadamu (Human Sexuality and Responsibility HSR) utafundishwa msimu huu wa Majani kupukutika (Fall) wakati wa darasa la afya la mtoto wako. Masomo hayo 9 yanashughulikia habari ya kukua na inayofaa kwa umr inayohusiana na uchumba na mahusiano ya kimapenzi, biashara haramu ya binadamu na usalama mtandaoni, anatomia ya uzazi na ujuzito, lezi na masuala ya kuthibisha babamipaka na kujizuiana ngono, afya ya ngono na kukaa salama, na ujuzi wa ridhaa na kukatabi. Mtaala huu umeanzishwa ili kutoa habari na ukuzaji ujuzi kwa wanafunzi ili waweze kufikia uwezo wao wa juu zaidi wa afya ya kimwili, kihisia, kiakili na kijamii.

Iwapo bado hujafanya hivyo, tunakualika ukague mtaala mtandaoni at <https://www.austinisd.org/pe-health/health-education/hsr> (chini ya kitufe cha KHS Lessons). Kama mwalimu mkuu katika maisha ya mtoto wako, AISD inaamini kwamba wewe ndiye chanzo muhimu zaidi cha habari kuhusu ujinsia wa binadamu. Mtaala wa HSR unakusudiwa kusaidia kile ambacho wanafunzi wanajifunza nyumbani, kuheshimu maadili ya familia yako binafsi na kuwafundisha wanafunzi kuheshimu maadili ya familia ya wengine ambayo huenda yakatofautiana na yao wenyewe.

Una haki ya kuamua kama mtoto wako atashiriki katika masomo haya. Ikiwa uchagua mtoto wako asishiriki katika moja au zaidi ya masomo haya, kutakuwa na masomo mbadala, yanayozingatia ujuzi wa kujifunza kijamii na kihisia, inayoandaliwa katika eneo tofauti.

Maelezo yote kuhusu sera ya HSR, muhtasari wa somo kwa kiwango cha darasa, nyenzo za familia, na zaidi yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya HSR: <https://www.austinisd.org/pe-health/health-education/hsr>. Ikiwa una maswali au wasiwasi wowote, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako au mkuu wa chuo.